

# UKEKETAJI WA WANAWAKE:

## desturi ya kuacha kabisa

*Uenyekiti wa Baraza la Mawaziri
na Wizara ya Nafasi Zilizo Sawa*

# UKEKETAJI WA WANAWAKE:

## desturi ya kuacha kabisa

Wapendwa Wazazi,

Ukeketaji wa wanawake ni kitendo cha zamani, kisicho halali au kisicho kubalika na dhehebu yo yote, na kimeshtumiwa katika mataifa mengi ya ulimwengu.
Kitendo hiki husaababisha mateso mabaya na mikwaruzo isioweza kurekebishwa kwa maisha yote ya wale ambao hukipitia kitendo hiki.
Unastahili kujua kuwa wakati msichana anapokeketwa, afya yake imo kwenye hatari ya shida kali za kiafya, na wazazi wanawajibika kisheria kuhukumiwa vikali sana katika taifa letu na katika mataifa mengine ya EU.
Wewe, mzazi, unastahili kujua kuwa hakuna uwajibikaji, hitaji, kusudi au faida ya kuwapitisha wasichana wako kwa kitendo hiki, ambacho kinahukumiwa pia na sheria.
Sababu ya watu wengi kuendelea na kitendo hiki bado haijulikani.
Inaaminika kuwa wanaheshimu kwa upofu desturi ya zamani bila kujiuliza wenyewe ni kwa nini.
Mwanzo wake unaweza kufuatiliwa hadi kwa kipindi cha Mafarao wa Misri.
Kutoka hapo ilienea katika mataifa mengi ya Kiafrika, ikichukua maumbile tofauti katika maeneo tofauti.
Tunaamini kuwa njia nzuri ya kuwajumuisha wageni ambao wamechagua kuishi katika nchi yetu ni kupitia mazungumzo na

uhamasishaji wa kawaida.
Kwa hivyo, tunahisi ni vyema kufafanua, kupitia pia kijikaratasi hiki, ya kuwa kuna haki ambazo Italia na jamii ya kimataifa inazingatia kuwa haziwezi kukeukwa, ikihusisha haki ya uadilifu wa kiakili na kimwili.
Tunaelewa kuwa inaweza kuwa ni vigumu kuachana na desturi ya zamani, lakini amini kuwa unajali kuhusu afya na furaha ya wasichana wako ambao wanahatarishwa kuwa chini ya desturi ambayo itaweka alama ambayo haiwezi kuondolewa katika miili yao na mioyo yao.
Wasichana wako wataishi katika milenia mpya, katika Italia kama raia wa Italia.
Tuwasaidie wakabiliane na maisha ya usoni wakiwa na tumaini na tabasamu.

Wizara ya Nafasi Zilizo Sawa



# MAJADILIANO YALIYOTOLEWA KWA AJILI YA UFYATAJI HAYAWEZI KUTETEWA

Kwa karne nyingi sababu nyingi tofauti, zimetolewa ili kutetea uendelezaji wa ukeketaji wa wanawake,zingine zabishana.
Zinapitana kidogo kati ya watu na maeneo ya kijeografia, lakini misingi ya sababu hizi zote ni dini au imani ya ushirikina, tamaduni na desturi.

Sababu zinazopeanwa sana sana ni hizi zinazofwata:

1. Ni kitendo cha kidini.
***Kuran, Biblia au Injili haipeani amri ya ukeketaji wa wanawake. Kati ya madhehebu mbali mbali, kuna maoni mengi yanayoongezeka ambayo yameinuka ili kuimarisha kuwa imani haihusiki katika vitendo hivi.***

2. Inaendeleza desturi.
***Desturi inategemea marekebisho yanayoendelea kwa jamii kwa mabadiliko ya kijamii na kihistoria. Hii pia ni kweli kwa ukeketaji wa wanawake.***
***Kwa kuachana na desturi hizo, mwanamke hasaliti desturi yake***



***mwenyewe, bali anaimarisha uhusiano ambao msingi wake ni imani mpya, kama vile haki za binadamu, maadili na uhuru wa mwanamke wa kuchagua.***

3. Ni kaida ya maana ya mwanzo.
***Kazi ya kaida ya mpito inapotea kila mahali. Siku takatifu na karamu ambazo hakuna damu inayomwagwa, kwa amani inahakikisha jamii inagundua mpito wa utu uzima.***

4. Ni safi
***Kinyume chake, inasababisha maambukizo mengi ya sehemu nyeti na mkojo. Ndiposa uweze kutunza usafi, kwa urahisi oga kila mara.***

5. Ni ujumi
***Wazo la umbo la mwanasesere, sehemu nyeti zilizo sawasawa ni wazo la kitamaduni ambalo halina udhibitisho katika ukweli.***

6. Ufyataji unahitajikana ili kutunza ubikra
***Sio kweli kwa sababu inaweza kutengenezwa tena baada ya kuingiliana (ufyataji tena). Badala yake, ni elimu iliyopokewa na imani ya mtu binafsi ambayo huongoza chaguo za kingono.***

7. Huongeza tamaa ya ngono ya mume wake.
***Sio kweli kwa sababu imedhibitishwa kuwa tamaa ya ngono ya mwanaume huongezeka ikiwa mwanamke ataonyesha hisia. Badala yake, kuingiliana kingono inakuwa uchungu kwa wanawake ambao wamekeketwa na inakuwa vigumu kwa wanaume kuingia.***

8. Inazuia tabia mbaya za ngono.
***Sio kweli kwa sababu haiwakomeshi wanawake kutokana na kuhusika katika vitendo "visivyofaa".***

## MAANA YA UKEKETAJI WA SEHEMU NYETI

Kuna aina tofauti tofauti ya ukeketaji wa wanawake, zote zinamadhara, na zinaweza kuwekwa katika vitengo vya:

***Kutahirishwa kisuna*** ambayo utekelezwa kwenye kinembe;

***Klitoridektomi*** ambayo kinembe chote ukatwa;

***Ufyataji*** ambayo sehemu nyeti za nje hukatwa na kitundu cha sehemu nyeti hushonwa ili kuruhusu mkojo na damu ya hedhi kupita peke yake;

Kuna vitendo vingine pia, ambavyo havijafafanuliwa kabisa, ambavyo ni hatari kwa sehemu nyeti za mwanamke.



## MADHARA KWA AFYA YA MSICHANA

Wazazi wapendwa, unastahili kugundua kuwa madhara ya vitendo hivi kwa afya ya kiakili na kimwili ya msichana wako inaweza kuwa kali sana. Haijalishi aina ya ukeketaji, ni nani aliyeitekeleza na ilikuwa chini ya hali gani ya usafi, kila wakati ina dhoofisha na ni dhuluma ambayo itadumu kwa maisha yote ya msichana wako, na katika kesi zingine inaweza kusababisha kifo.

**Kwanza kabisa, unastahili kujua kuwa ufyataji, wa aina yo yote, sio kitendo cha kupuuzwa, bali operesheni ya gainekolojia wa kweli. Kupasuliwa ambao gainekolojia anastahili kufanya ambao hakufanywi hospitalini na gainekolojia (au daktari wa upasuaji) huweka maisha ya mgonjwa hatarini.**

Wakati ukeketaji huu unafanywa bila unusukaputi na bila uhakikisho kutoka kwa daktari wa upasuaji, wasichana mara kwa mara **hupoteza fahamu na kushtuka**, kwa sababu ya uchungu mwingi unaosababishwa na kupasuka kwa sehemu nyeti na vidonda **kutoa damu.** Kutokwa na damu, ambayo ndiyo hutendeka sana na madhara ya mara kwa mara ya operesheni hii, haiwezi kuhepukika. Kwa kweli, unastahili kujua kuwa kinembe, ambacho hukatwa, ni mojawapo ya sehemu ya utomvu ya mwili. Kama umwagikaji wa damu hautasimamishwa kwa wakati mzuri, msichana anaweza kufa. Na hata pia kama damu haimwagiki nyingi, kupoteza damu kunaweza kuendelea kwa masiku, ambayo inaweza sababisha hali ya anemia. Lakini sio madhara ya muda mfupi peke yake. Hata ikiwa damu kupotea inaweza kudhibitiwa, bado kuna hatari ya kidonda kuambukizwa.

***Maambukizo*** husababishwa na ukosefu wa hali ya usafi inayotakikana na operesheni zote za upasuaji. Uchungu haukomi papo hapo baada ya operesheni.
Wasichana huteseka hadi mahali ambapo hawataki kukojoa kwa masiku baada ya operesheni kwa sababu ya uchungu mwingi.
Kukosa kukojoa husababisha shida ya kiafya iitwayo ***uzuiaji mkojo.***
Kwa hivyo, eneo la kukojoa huambukizwa hivyo basi kuongezea hatari zaidi kwa afya ya msichana.
Maambukizo uenea kwa ogani zilizo karibu, kama vile njia ya mkojo, sehemu nyeti, rektamu na kadhalika.



Kando na maambukizo ya kawaida, ambayo mara kwa mara huanza kukidhiri na kubadilika na kuoza, unastahili kujua kuwa msichana anaweza kufa kutokana na ***pepopunda*** kwa sababu ya kutumiwa kwa vifaa ambavyo havikuwa vimesafishwa, na kutokana na ***HIV/UKIMWI au homa ya manjano*** kwa sababu ya kurudia kutumia vifaa vile vile.

Ikiwa msichana ataponea operesheni hiyo, wakati atakapokuwa mtu mzima anaweza kuteseka mfululizo safu ya **"*muda mrefu*"** ya kudhoofika na magonjwa.Hizi zinaweza kuwa shida kubwa za kiafya ambazo hufupisha uzuri na urefu wa maisha yake .

Kati ya hizi, zile za mara kwa mara ni:

***Ugumu wakati wa kukojoa:*** Inayosababishwa na mahali pa kukojoa kuzuiliwa au eneo la kukojoa kudhoofika.
Kukojoa kunaweza kuwa na uchungu, na kwa hivyo, wanawake hawa hawakojoi sana. Hii husababisha shida za kiafya kwa mfumo wa kukojoa, sana sana zile zinahusiana na kuambukizwa.



***Kuambukizwa maradhi ya muda mrefu, yanayoendelea na kuenezwa katika sehemu nyeti na ogani za uzazi za ndani.***

***Ugumu wa kupata watoto (tasa):*** Kwa kawaida kwa sababu ya kuambukizwa ambao kunaweza kusababisha madhara yasiyoweza kutibiwa kwa ogani za uzazi.

***Vidonda vya kweli kwa sehemu nyeti (Keloidi):*** Muundo huu mara kwa mara hufunga kitundu cha sehemu nyeti na kufanya iwe vigumu kuingiliana kingono na kufanya iwe vigumu kwa damu ya hedhi kupitia kitundu chake cha asili.

***Shimo au majeraha kati ya sehemu nyeti na kibofu cha mkojo au kati ya sehemu nyeti na rektamu (fistula).***

Katika kesi hizi wakati mwingine mkojo na kinyesi hupitia kitundu kimoja.

***Uchungu wakati wa kuingiliana kingono*** ni madhara ambayo hayawezi kuzuiliwa, itakuwa kawaida kwa wanawake hawa wasio na bahati. Wakati mwingine kuingia kwa ogani ya ngono ya mwanaume ni vigumu au haiwezi kuingia, na kwa kesi zingine upasuaji uwezeshwa ili kuwezesha kuingiliana kingono.

Lakini hata pia kwa wanawake wale ambao wamekeketwa, haijalishi kitu cho chote wameweza kuzaa, ***shida hutokea tena wakati wa kubeba mimba na kuzaa:*** Ni jambo la kawaida kwa wanawake ambao wameteseka udhoofu wa aina hiyo. Kidonda kinaweza kuzuia kupanuka kwa njia ya kuzaa na kuzuia uchungu wa kuzaa.
Halafu kuna mfululizo safu mwingi wa kudhoofika kutokana na kutengenezwa kwa ***ujumuishaji kwa kilengelenge katika sehemu nyeti*** (kilengelenge kilichosababishwa na kujumuishwa kwa vipande vya vitu kwa kidonda) Wakati mwingine fungu la tishu la neva uundwa kwenye mkato (***Neuroma***), ambapo neva ya kinembe kimekatwa. Eneo lote la sehemu nyeti linakuwa nyepesi kuhisi na husababisha uchungu usioweza kuvumiliwa na wa kila mara.

## JE NI NINI KITAKACHOTOKEA HAPA ITALIA IKIWA MTOTO WA KIKE ATATAHIRIWA?

Sheria mpya iliyopitishwa na Bunge hivi karibuni imeeleza kuwa ukeketaji wa viungo vya uzazi vya wanawake kuwa ni kosa la jinai.

Hasa, muda wa vifungo unakuwa kuanzia miaka minne hadi kumi na mbili kwa wale wanaojihusisha na ukeketaji wa viungo vya uzazi vya wanawake.

Ukeketaji wa viungo vya uzazi vya wanawake unajumuisha ukataji wa sehemu ya juu ya kinembe, ukataji wa kinembe chote, kuifanya finyu sehemu ya kuingilia ukeni na vitendo vingine vinavyoleta madhara yanayofanana.



Muda wa vifungo kwa kusababisha majeraha mengine kwenye sehemu za siri za mwanamke(mbali na yale yaliyotajwa hapo nyuma) na magonjwa ya kimwili na kiroho unakuwa kuanzia miaka miaka mitatu hadi saba. Hukumu hupunguzwa kwa theluthi moja ikidhihirika kuwa majeraha ni madogo.

Adhabu huongezwa kwa theluthi moja ikiwa vitendo hivi husababisha madhara kwa mtoto,kisheria,au vikifanyika kwa nia ya kujipatia faida kutokana navyo.

Vifungu hivi pia vinatumika ikiwa vitendo hivi vimefanyika nje ya nchi na raia wa Italia au wageni wanaoishi Italia au wakati madhara yanafanywa kwa raia wa Italia au mgeni anayeishi Italia.



## HITIMISHO

Ufyataji, kama vile ukeketaji wote wa sehemu nyeti, husababisha madhara kwa wasichana wako.
Vitendo hivi vimeshtumiwa na maserikali mengi ya ulimwengu na hata pia Shirika la Afya la Dunia.
Katika taifa letu wanahukumiwa vikali sana kwa sheria ya uhalifu.
Ni desturi ambazo zinasababisha uchungu na mateso kwa wale ambao huyapitia na ni lazima yakandamizwe kabisa kwa uzuri wa wasichana wako.
Miundo ya afya na ushauri wa kijamii na hata pia mashirika ya wanawake wahamaji yanapatikana kwa ajili yako ukitaka kuzungumza nao, ukitaka mashauri na usaidizi kuhusu mambo haya.
Kwa hivyo tunakukaribisha uweze kwenda kwa kizio cha afya cha mtaani au kituo cha mashauri ya jamii ikiwa unahitaji maelezo yo yote zaidi au usaidizi.
Kwa maelezo zaidi, shauriana na tovuti ya Wizara ya Italia ya Nafasi zilizo Sawa: www.pariopportunita.gov.it





Imetayarishwa pongezi kwa mchano wa kisayansi
Wa Daktari Arro Hersi Magan
na Profesa Claudio Giorlandino
na pia Ukumbi wa Jumuiya ya Wageni

www.pariopportunita.gov.it

Huu ni mpango kutoka kwa:

*Uenyekiti wa Baraza la Mawaziri*
*na Wizara ya Nafasi Zilizo Sawa*

Kwa kushirikiana na:

*Wizara ya Afya*

*Wizara ya Mambo ya Nje*

*Wizara ya Mambo ya Ndani*

*Wizara ya Elimu,*
*Vyuo Vikuu na Utafiti*

*Uenyekiti wa*
*Baraza la Mawaziri*

MKUTANO WA KUDUMU WA UHUSIANO BAINA YA NCHI,
MIKOA NA MIKOA INAYOJITEGEMEA
YA TRENTO AND BOLZANO

*Wizara ya Kazi na*
*Sera za Jamii*